




**Uchambuzi wa Taarifa za Mlinganisho wa Mapato yanayotokana na Sekta ya Uziduaji:  
Mchango wake katika Maendeleo ya Taifa kati ya Mwaka 2009 hadi 2019**

**Uchambuzi wa Kiseru**



## Shukrani

HakiRasilimali (wachapishaji) inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa kila mtu ambaye alishiriki katika kuandaa na kukamilisha ripoti hii kwa utalam wao, muda, utayari, nguvu na ushirikiano katika kutekeleza na kukamilisha ripoti hii. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Bwana Moses Kulaba na Bi Beatrice George (waandishi) kwa juhudi zao za pamoja katika kutafiti na kuandika ripoti hii.

HakiRasilimali pia inashukuru taasisi zote na watu binafsi walioshiriki wakati wa ukusanyaji wa data na kukagua rasimu ya ripoti hiyo. Maoni yao yamekuwa muhimu katika uundaji wa ripoti hii.

HakiRasilimali inashukuru wanachama wake, ambao wametoea msaada mkubwa wakati wa kufanya utafiti huu. HakiRasilimali pia inashukuru wafanyikazi wake wa Sekretarieti, ambao wametoea msaada wa vifaa na kiutawala wakati wa kufanya utafiti.



# Table of Contents

<b>1.0 Introduction and Background.....</b>	<b>1</b>
1.1 Specific Objectives of the study.....	1
1.2 Methodology & Execution strategy.....	1
<b>2.0 Contextual background.....</b>	<b>2</b>
2.1 Conceptualization of transparency chain in Extractive Sector.....	2
2.2 Tanzania’s extractive sector and revenue regulatory framework .....	2
<b>3.0 Revenue Disclosure Trends.....</b>	<b>4</b>
<b>4.0 Contribution to the economy.....</b>	<b>6</b>
4.1 Contribution to Employment.....	9
<b>5.0 Non Fiscal Benefits .....</b>	<b>12</b>
5.1 Extractive sector contribution to local Procurement of Goods and Services.....	13
<b>6.0 Contribution of Energy Sector .....</b>	<b>15</b>
<b>7.0 Reporting of State Participation .....</b>	<b>17</b>
<b>8.0 Government response and implementation of recommendations .....</b>	<b>19</b>
<b>9.0 Role of CSO and Policy Actors .....</b>	<b>19</b>
<b>10.0 Key Gaps.....</b>	<b>21</b>
<b>11.0 Recommendations to major stakeholders.....</b>	<b>28</b>
<b>12.0 References .....</b>	<b>30</b>
<b>13.0 Glossarium of key extractive Sector Revenue terms.....</b>	<b>31</b>



---

## 1.0 Utangulizi

---

HakiRasilimali, mtandao wa asasi za kiraia uliojikita katika kuchagiza uwazi na uwajibikaji kwenye sekta ya uziduaji, imefanya uchambuzi wa ripoti za mlinganisho wa mapato ya sekta kama yalivyoriipotiwa na Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji Tanzania (TEITI). Uchambuzi huu unatumia taarifa rasmi zilizotolewa na TEITI katika kipindi cha miaka 10 iliyopita; yaani kuanzia Julai 2008/2009 hadi Juni 2018/2019. Malengo makubwa ya uchambuzi huu ni kutaka kujua mchango wa sekta ya uziduaji katika kusaidia maendeleo ya Tanzania na pia kuchochea utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa na Mpango wa Uhamasishaji wa Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji (EITI) na TEITI hapa nchini. Pamoja na yote, jambo la muhimu zaidi katika uchambuzi huu ni kujaribu kuibua mjadala mpana kuhusu uwazi na uwajibikaji kwenye matumizi ya mapato yanayotokana na sekta ya uziduaji hapa Tanzania.

Tanzania ilijiunga na EITI mnamo Februari mwaka 2009 na ikatangazwa kukidhi viwango vya EITI mnamo Desemba 2012. Kukidhi kwa viwango vya EITI kulipelekea Tanzania kuweza kupitisha Sheria ya Sekta ya Uziduaji (Uwazi na Uwajibikaji) ya mwaka 2015 (Sheria ya TEITA). Kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo zilitungwa mnamo mwaka 2020.

Pamoja na mambo mengine, sheria hiyo ilipendekeza kuundwa kwa chombo maalumu (Multi Stakeholders Group au MSG) kinachoundwa na makundi matatu ya wadau muhimu katika sekta hiyo katika kuchagiza uwazi na uwajibikaji kwenye sekta. Makundi haya yanaundwa na wawakilishi watano kutoka kwa kila mdau; Serikali, Kampuni za Uziduaji na Asasi za Kiraia; zikiongozwa na Mwenyekiti anayeteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati hii ya wadau hufanya kazi ya uangalizi kwenye kuhakikisha kwamba viwango vya EITI pamoja na sheria ya TEITA vinafuatwa na kutekelezwa – huku dhumuni la kuhakikisha kuna uwazi na nchi kufaidika na mapato ya sekta hii pia likitimizwa.

Mojawapo ya sababu zilizoichochea Tanzania kujiunga na EITI, pamoja na mambo mengine, ilikuwa ni kuifanyia mabadiliko sekta ya uziduaji na kuifanya iwe na faida zaidi ili kwamba nchi ifaidike na mapato yanayopatikana kutoka katika sekta za madini, mafuta na gesi. Ni matakwa ya EITI katika ngazi ya kimataifa kwamba nchi zote zilizo wanachama, ikiwamo Tanzania, ziweke utaratibu wa kuweka hesabu zake rasmi za mapato hadharani, kwa kampuni kusema zimelipa nini kwa serikali na ushahidi wa risiti za malipo hayo kwa kila mwaka wa fedha wa serikali. Mchakato huo hutakiwa kufikia vigezo vyote vilivyowekwa na Kamati ya TEITI na taasisi za serikali (STAMICO na TPDC) na kampuni binafsi za uziduaji zikitakiwa kufuata mwongozo uliowekwa.

Ripoti za TEITI huandaliwa na mkaguzi huru wa hesabu ambaye naye huwa chini ya uangalizi wa wadau wa sekta ya uziduaji kwenye mwamvuli wa MSG.

Katika kukidhi lengo hili, uchambuzi huu uliofanywa kwenye hesabu hizi za mapato yaliyokaguliwa na TEITI unatoa picha yakinifu ya hali halisi – ukiangazia katika masuala anuai kama vile uwazi kwenye kuonyesha mapato, mchango kwenye uchumi, vyanzo kinara vya mapato, mchango kwenye ajira, mchango wa wachimbaji wadogo, faida zisizo za kikodi, ushiriki wa serikali/dola, mrejesho kutoka serikalini na utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa kwenye ripoti hizo za TEITI.

---

## 2.0 Faida Kuu za Kuripoti Mahesabu ya TEITI

---

Kuongezeka kwa uwazi na upatikanaji wa taarifa kuhusu mapato ya sekta ya uziduaji; ikionyesha tofauti au kutoendana baina ya kile ambacho kampuni za madini na gesi asilia zinatoa taarifa kuwa zimelipa na kile kilichopokewa na serikali. Hadi sasa, kiwango kikubwa zaidi cha tofauti kati ya kinachodaiwa kulipwa na makampuni na kile kilichopokewa na serikali kimeonekana katika ripoti ya saba na nane ya TEITI ambako tofauti ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 27 na bilioni 30.5 mtawalia.

Zaidi, ripoti za TEITI zimeweka bayana maeneo hatarishi kwa upotevu wa mapato kwa kuandikwa ndivyo sivyo, rushwa na ukwepaji wa kodi. Kwa mfano, pasipo na shaka yoyote, kama ripoti za TEITI zisingekuwapo, kiwango hicho kinachotajwa kama tofauti, huenda kisingeripotiwa popote. (Tazama jedwali la kwanza).

Uwazi katika mapato na malipo kumejenga mazingira wezeshi kwa uwekezaji, kutengeneza kuaminiana na jamii/wadau kwenye maeneo ya uwekezaji na pia kutoa kibali cha kukubalika kwenye jamii kwa kampuni za uziduaji kufanya shughuli zao.

Utekelezwaji wa viwango vya EITI hapa Tanzania umechagiza kuwepo kwa mijadala kwa wadau iliyosaidia kuanza kwa malipo ya kodi ya mapato na huduma ambayo yamefanywa na kampuni za uziduaji kwenye halmashauri ambako kampuni hizo zinaendesha shughuli zake na kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kwa mfano, ripoti ya TEITI ya mwaka 2009/10 ilibainisha kwamba kiasi cha asilimia 0.3 kama tozo ya huduma iliyolipwa na kampuni ya PanAfrican Energy Tanzania inayofanya kazi zake eneo la SongoSongo Kusini mwa Tanzania, kililipwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam ziliko ofisi za kampuni hiyo badala ya Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inakochimbwa gesi hiyo. Tangu jambo hilo kuwekwa wazi, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi imekuwa ikipokea wastani wa shilingi milioni 110 (dola 61,000) kila robo mwaka ikiwa kama tozo ya huduma. Mwaka 2016 kulikuwa na mijadala mikali kuhusu malipo ya kodi ya mapato kwa kampuni za uziduaji zinazofanya kazi zake nchini Tanzania kwa muda mrefu. Mijadala hiyo ndiyo yaliyosababisha serikali na kampuni ya Acacia kufanya mapitio ya malipo ya kodi ya mapato kwa kampuni hiyo. Kupitia majadiliano hayo, Acacia ilikubali kufanya malipo ya kodi ya mapato ya kiasi cha dola milioni 14 za Marekani<sup>1</sup>.

---

<sup>1</sup><http://www.acciamining.com/~-/media/Files/A/Acacia/press-release/2016/first-quarter-results-2016-pr.pdf>

**Jedwali: Tofauti baina ya kinachodaiwa kulipwa na kilichopokewa 2008-2018**

S/N	Mwaka wa kuripoti	Idadi ya makampuni	Malipo Yaliyoripotiwa na Makampuni	Malipo Yaliyoripotiwa na Serikali	Tofauti ya Malipo (Kiasi)	Tofauti kwasilimia
1	2008/09	11	62,151,063,000	38,035,600,000	24,115,463,000 <i>-Final 2.1bln &amp; USD 328,865)</i>	6.3%
2	2009/10	23	424,554,440,000	419,552,271,000	5,002,169,000	1%
3	2010/10	29	508,246,317,384	497,246,612,897	10,999,704,488 (11bln)	2.21%
4	2011/12	43	759,817,251,440	757,668,713,459	2,148,537,981	0.28%
5	2012/13	65	947,317,664,855	956,165,169,391	8,847,505,536	0.93%
6	2013/14	59	1,218,787,045,379	1,221,215,617,951	2,428,512,571	0.20%
7	2014/15	31	337,811,375,708	311,250,624,831	27,090,667,583	8.7%
8	2015/16	55	465,164,747,725	434,627,874	30,536,873,35	7%
9	2016/17	70	510,610,821,731	508,624,111,294	1,986,710,437	0.39%



### 3.0 Mchango Katika Uchumi


---

Ripoti za mahesabu za TEITI zimeonyesha kwamba ukubwa wa mchango wa sekta ya uziduaji kwenye uchumi wa Tanzania kupitia Pato la Taifa (GDP). Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 mchango wa sekta hii ulifikia kiasi cha shilingi 4,975,991,000,000 na kuongezeka kufikia kiasi cha shilingi 5,206,217,000,000 mwaka 2017, na kuongezeka kwa asilimia 5.08 mwaka 2018 kufikia kiasi cha shilingi 6,573,059,000,000. Mchango wa sekta ya uziduaji kwenye Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 3.2 mwaka 2010/11 hadi asilimia 4.8 mwaka 2017/18. Kwa ujumla, mchango wa sekta hii umekuwa mkubwa na thabiti katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Yakini, sekta ya madini imechangia asilimia 85 ya mapato yote ya sekta ya uziduaji katika mwaka 2015/2016 na asilimia 79.69 mwaka 2016/17 kabla haujapungua kidogo mwaka 2017/2018 kwa kuchangia asilimia 75.84 ya mapato yote ya sekta ya uziduaji. Mapato yanayotokana na sekta ya mafuta na gesi yameongezeka pia kwa kiasi kikubwa; kutoka asilimia sita ya mapato yote mwaka mwaka 2014/2015 kufikia asilimia 15 mwaka 2015/2016. Mwaka 2017/18 sekta hiyo pia ilikua kwa asilimia tisa kiasi cha kuweza kuchangia asilimia 24.17 ya mapato yote ya uziduaji. Kwa ujumla, sekta ya gesi imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia tisa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Taarifa za mchango wa sekta ya mafuta na gesi zitajadiliwa kwa kina chini. Pamoja na mafanikio hayo, sekta ya uziduaji bado inaandamwa na changamoto kadha wa kadha.

#### **Matokeo:**

- Hakuna maelezo ya kutosha kuhusu ni kwa vipi pamoja na ukuaji huu wa sekta ya uziduaji bado mchango wake kwenye GDP umebaki kuwa mdogo (kwa asilimia 3.2 hadi 4.8) na kudumaa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2015/2018). Katika mazingira ya kawaida, mchango wa sekta hii ulipaswa kuwa mkubwa na unaoongezeka kila mwaka kwa sababu mapato zaidi yanakusanywa huko. Uchambuzi huu wa kina unaonyesha kwamba takwimu hizi zimebaki kuwa karibu vilevile katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Kutoka katika ripoti za TEITI, mchango wa sekta ya uziduaji mwaka 2012/13 ulikuwa asilimia 11.91 ya mapato yote ya kifedha ya serikali; ikiongezeka kutoka asilimia 11.9 mwaka 2011/2012. Hata hivyo, ripoti za karibuni zinaonyesha mchango wa sekta hiyo umeshuka kufikia asilimia moja ya mapato yote ya kifedha. Je, hii maana yake ni kwamba mchango wa sekta ya uziduaji kwenye mapato ya serikali umepungua kwa maana ya asilimia katika miaka ya karibuni au mapato ya serikali yasiyo ya kodi yameongezeka?
  - Makusanyo ya asilimia moja ya mapato yanayokusanywa na halmashauri kunakofanyika uziduaji yanaonyesha kwamba kiasi kikubwa cha fedha hizo huchukuliwa na Serikali Kuu kupitia wakala wake kama TRA, Wizara ya Madini na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Hii imeanza kuzua wasiwasi kwamba sasa halmashauri ambako kunakofanyika uziduaji zimeanza kupoteza mapato haya muhimu yanayotokana na utajiri uliopo kwenye maeneo yao.
-



Jedwali 3: Jedwali hili linaonyesha ukuaji wa sekta ya uchimbaji madini kwa kuzingatia bei za mwaka 2007, mchango kwenye GDP kwa bei za sasa na mapato ya uzidujaji yaliyowekwa wazi kati ya mwaka 2008-2018. \* Takwimu kuhusu asilimia ya mchango wa madini kwenye GDP ni za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na taarifa za mapato zinatokana na ripoti za mahesabu za TEITI. \*\* Kuna tofauti kidogo kwenye taarifa za BoT na zile za TEITI. Kuna umuhimu wa kuweka mfumo mzuri wa kukusanya na kuhifadhi taarifa rasmi za serikali.

- Uzalishaji wa madini nchini Tanzania umeongezeka kutoka shilingi trilioni 2.2 mwaka 2009 hadi shilingi trilioni 4.78 mwaka 2016. Hata hivyo, thamani ya uzalishaji imeshuka kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.01 kutoka shilingi trilioni 4.78 mwaka 2016/2017 hadi shilingi trilioni 3.77 mwaka 2017/18. Thamani ya uzalishaji wa madini imeongezeka kutoka shilingi trilioni 2.2 mwaka 2009 hadi shilingi trilioni 4.78 mwaka 2016. Hata hivyo, katika kipindi cha kati ya mwaka 2016/17 na 2017/18, thamani hiyo ilishuka kwa kiasi cha shilingi 1.01 kutoka shilingi trilioni 4.78 hadi shilingi trilioni 3.77. Thamani ya madini yaliyouzwa nje ya nchi iliongezeka kufikia dola za Marekani 2,145,000,000 mwaka 2016 lakini kiasi hicho kilipungua kwa asilimia 10.8 kutoka dola za Marekani 1,860,200,000 hadi dola za Marekani 1,695,000,000 mwaka 2017/18. Thamani ya mauzo ya madini nje ilishuka kwa kiwango cha asilimia 13.3 kati ya mwaka 2016 na 2017. Sababu kubwa ilikuwa ni mabadiliko yaliyofanywa katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na mwaka 2017 mabadiliko ya sheria yalipiga marufuku usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi na kuchagiza uongezaji thamani wa madini ndani ya nchi.



Jedwali namba 4: Grafu inayoonyesha mwenendo wa uzalishaji madini na thamani ya uzaji nje ya nchi (2015-2018)




## 4.0 Mchango Kwenye Ajira

Kwa mujibu wa takwimu za karibuni kupitia Utafiti wa Kipato Kupitia Ajira Rasmi (FEES) unaofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kama ulivyonukuliwa katika ripoti ya tisa ya TEITI, sekta ya uchimbaji inayojumuisha madini na mawe, imeajiri takribani watu 35,900 ikijumuisha waajiriwa wa moja kwa moja na vibarua. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 1.4 ya idadi ya watu wote wanaofanya kazi hapa nchini. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko dogo la asilimia 1.3 kutoka idadi ya wafanyakazi na vibarua 30,259 mwaka 2015<sup>2</sup>.

### Matokeo:

- Kulinganisha na idadi ya wafanyakazi katika sekta ya uziduaji, mchango wao katika uchangiaji wa mapato ya taifa ni mkubwa. Mwaka 2008/09, michango ya kodi ya mapato ya wafanyakazi wa sekta ya uziduaji kwenye uchimbaji pekee ilikuwa sawa na asilimia 48.74 ya michango ya jumla ya sekta nzima. Mwaka 2010/11, michango hiyo ilifikia kiwango cha asilimia 23 ya mapato yote ya uziduaji. Mapato ya Kodi ya Mshahara (PAYE) yaliyokusanywa na TRA kutoka kwenye kampuni za uziduaji yalifikia kiasi cha shilingi 141,783,098,832 (shilingi bilioni 142) ambayo ni sawa na asilimia 20.6 ya mapato ya jumla ya sekta hii.

**Mchango wa mapato yatokanayo na ajira za sekta ya uziduaji kwa kipindi cha miaka ya karibuni kama yalivyochukuliwa kutoka ripoti za TEITI za miaka ya nyuma.**



- Takwimu hizi zinaonyesha kwamba sekta hii haitengenezi ajira nyingi ipasavyo kulinganisha na mahitaji na hivyo serikali ina fursa ya kujenga mazingira yatakayoongeza ushiriki wa wananchi katika uchimbaji mdogo wa madini miongoni mwa wachimbaji watanzania, vijana na wasio na ajira.

<sup>2</sup>TEITI: The 9th TEITI Report for the period July, 1, 2016 to June, 30th, December 2019

---

## 5.0 Mchango wa Wachimbaji Wadogo

---

Kwa mujibu wa ripoti ya saba ya TEITI, mwaka 2014 Tanzania ilikuwa na wachimbaji wadogo wa madini 600,000 na hivyo kuifanya kuwa sekta iliyoajiri watu wengi zaidi hapa nchini. Hata hivyo, katika ripoti za TEITI eneo hili la wachimbaji wadogo wa madini na migodini huwa halitazamwi kwa kina.

### **Matokeo:**

- Taratibu, serikali imeanza kutambua mchango mkubwa wa wachimbaji wadogo wa madini katika uchumi wa taifa. Kufikia mwaka 2019, serikali ilikuwa imetenga maeneo 11 yenye ukubwa wa jumla wa hekta 38,952 kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini. Serikali pia ilianzisha vituo saba vya umahiri na mafunzo kwa wachimbaji wadogo ili kuwaongezea uwezo na tija kwenye kazi zao na pia imeanzisha masoko 28 kwa ajili ya kununua madini kutoka kwa wachimbaji na wauzaji wadogo. Serikali imeweka pia utaratibu na kupelekea wachimbaji hawa wadogo kufutiwa kodi ya zuio ya asilimia tano na pia hawatozwi Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya asilimia 18 wakati wanapouza madini yao kwenye masoko hayo yaliyotengwa na serikali.
  - Baadhi ya taarifa muhimu na mahesabu hayajawekwa vizuri na taarifa hizi zimepatikana tu kwa kuku-sanya taarifa zenye muktadha wa sekta ya uziduaji.
  - Katika nyakati tofauti za kutafuta taarifa kuhusu uchambuzi huu, watafuta taarifa huru walikosa taarifa muhimu za kitakwimu kutoka kwa wachimbaji wadogo kwa sababu wengi wao hawana utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu.
-


## 6.0 Faida Kutoka Mapato Yasiyotokana na Kodi

Kampuni za uziduaji zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii kwa kuchangia fedha kwenye miradi ya kuendeleza jamii za Kitzania kwa mujibu wa vigezo vya EITI.

### 6.1 Matokeo:

Ripoti za TEITI zinaonyesha kwamba mchango wa kampuni za uziduaji kwenye jamii kupitia michango isiyo ya malipo ya kodi imeongezeka kuanzia mwaka 2011/12 ambako zilichangia kiasi cha shilingi bilioni 29. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, mabilioni ya shilingi yamechangwa na kuwekezwa katika miradi ya kijamii kwenye maeneo mengi nchini Tanzania kutokana na fedha kutoka kampuni hizi.

#### a) Jedwali: Michango ya Kifedha 2017/18




Chanzo: Ripoti za TEITI



- Sekta ya elimu ilikuwa mfaidika mkuu wa mapato haya yasiyo ya kikodi kwa kupokea kiasi cha shilingi bilioni 9.7 mwaka 2016/17 na shilingi bilioni 6.6 mwaka 2017/18. Eneo lingine lililopata fedha nyingi lilikuwa ni miundombinu ikifuatiwa na miradi mingine ya kiuchumi na kijamii.
- Kampuni ya Geita Gold Mine ndiyo kinara wa kutoa mchango wa uwajibikaji kwa jamii kupitia njia hii, ikiwa imechangia kiasi cha shilingi bilioni sita mwaka 2017/2018 ikifuatiwa na kampuni ya North Mara ambayo ilichangia kiasi cha shilingi bilioni nne mwaka huohuo.

**MUHIMU:** Pamoja na kiasi hiki kikubwa cha fedha kilichotolewa kusaidia jamii, ripoti za TEITI hazionyeshi kwamba michango hii ni sawa na asilimia ngapi ya mapato ya jumla ya kampuni hizi kwa mwaka. Uwepo wa takwimu hizi ungesaidia sana kujua kama kiwango kinachotolewa kinaendana na kiasi kinachotarajiwa kutokana na viwango vya kimataifa vya sekta husika.

## b) Jedwali: Ununuzi wa Bidhaa na Huduma kutoka Nchini



Chanzo: Ripoti ya 10 ya TEITI kwa kipindi kinachoishia Juni 30, 2018

- Jedwali hili linaonyesha kuwa kampuni ya Pan African Energy ndiyo iliyotumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha kununua huduma na bidhaa kutoka ndani ya nchi; ikitumia kiasi cha shilingi bilioni 296.2 ikifuatiwa na kampuni ya Shanta Mining iliyotumia shilingi bilioni 165, Williamson Diamonds shilingi bilioni 127.5 na North Mara shilingi bilioni 115.1.

## 7.0 Mchango wa Sekta ya Nishati (Mafuta na Gesi)

Sekta za mafuta na gesi bado ni changa hapa Tanzania. Sekta hii bado haijafanikiwa kuzalisha mafuta lakini tangu mwaka 2004 imekuwa ikizalisha gesi asilia. Wazalishaji wakuu wa gesi asilia ni kampuni ya M&P Exploration (T) inayofanya shughuli zake katika eneo la Mnazi Bay na Pan African Energy Tanzania inayoendesha shughuli zake katika eneo la Songo Songo. Kufikia mwaka 2018, Tanzania ilikuwa na hifadhi ya gesi asilia kiasi cha futi za ujazo 57.54. Kiasi hiki bado hakijaanza kuvunwa kwa kina na bado kazi ya utafutaji wa maeneo mengi zaidi yenye gesi inaendelea.

Kwa mujibu wa ripoti ya 10 ya TEITI, uzalishaji wa kampuni hizi mbili za gesi asilia uliongezeka kutoka scf 47,456,860,000 mwaka 2017 hadi scf 59,142,000 mwaka 2018. Thamani ya gesi asilia iliyozalishwa iliongezeka kutoka kiasi cha dola za Marekani milioni 42.2 hadi kufikia dola za Marekani milioni 63.8 katika kipindi hicho-hicho. Kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji na thamani ya gesi asilimia kumechangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa hiyo viwandani na majumbani. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kiasi kikubwa zaidi hutumiwa na Shirika la Umeme la TANESCO kwa ajili ya uzalishaji umeme.

### Jedwali: Uzalishaji wa Gesi Asilia 2017/18

Kampuni	Eneo	Uzalishaji (Futi za Ujazo, Thamani (USD) Scf)			
		kwa '000'			
		2017	2018	2017	2018
<b>M &amp; P Exploration (T) Limited</b>	Mnazi Bay	17,960,300	30,405,160	19,466,121	40,683,088
<b>Pan African Energy Tanzania Limited</b>	Songosongo	29,496,560	28,736,840	22,795,142	22,406,171
<b>JUMLA</b>		<b>47,456,860</b>	<b>59,142,000</b>	<b>42,261,263</b>	<b>63,089,259</b>



---

**Mchango:**

- Ingawa kuna ongezeko kubwa la uzalishaji wa gesi asilia na mapato kutoka katika sekta hii ndogo ya mafuta na gesi, kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa nyaraka za kuonyesha ni kwa namna gani sekta hii inachangia katika maendeleo ya kiuchumi.
  - Kwa kutazama nyaraka zilizopo na ripoti hiyo ya mahesabu ya TEITI, mtu anaweza kupata picha ya kwamba mchango wa sekta hii kwenye uchumi ni mdogo ingawa ukweli ni kwamba imetoa mchango mkubwa katika uzalishaji wa umeme na uanzishwaji wa viwanda vingi hapa nchini.
  - Ripoti hizo 10 za TEITI hazijaonyesha kama kwenye uzalishaji wa gesi asilia kuna makinikia pia na kama yapo ni kiasi gani na kama yanasafirishwa nje ni kwa thamani gani. Mjadala huu ni muhimu kwa sababu ya mjadala uliojitokeza katika eneo la makinikia ya madini miaka michache iliyopita.
  - Katika ripoti za TEITI, hakuna mahali ambako kuna taarifa inayoonyesha (kutoka kampuni zinazovuna gesi asilia) kuhusu makinikia hii. Kwa mujibu wa vyanzo kutoka Sekretarieti ya TEITI na TPDC, kiasi na soko la makinikia ya gesi asilia kutoka Tanzania bado ni kidogo. Makinikia hii inaelezwa kupatikana zaidi kutoka Songosongo kuliko Mnazi Bay kutokana na tofauti ya miamba iliyopo kwenye vitalu vya maeneo hayo mawili. Mapato yanayopatikana kupitia mauzo ya makinikia haya yako nje ya mawanda ya kisheria ya Sheria ya Mapato ya Gesi na Mafuta ya mwaka 2015 na hayahusiki na TEITI. Mapato yatokanayo na makinikia haya huchukuliwa kuwa ni siri na huwekwa kama sehemu ya mapato ya TPDC.
  - **MUHIMU:** Kwa maelezo mafupi, makinikia ya gesi ni kimiminika kilicho ndani ya gesi asilia. Kwa kawaida hiyo, kimiminika hiki huuzwa tofauti na gesi na hupatikana wakati wa zoezi la kufua gesi. Kimiminika hiki, mara nyingi, hutumika kwa kuchanganywa kwenye vitu rahisi kulipuka kama mafuta wakati wa kuvisafirisha kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine au nje ya nchi. Kuchanganywa kwake kwenye mafuta huondoa uwezekano wa mafuta kulipuka wakati yakiwa yanasafirishwa kwa utaratibu mwingine isipokuwa bomba.
-



## 5.0 Ushiriki wa Serikali/Dola

---

Sheria na taratibu zinazoongoza sekta ya madini, gesi na mafuta nchini Tanzania zinaruhusu ushiriki wa dola katika biashara hiyo. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la Mendeleo ya Petrol Tanzania TPDC vina mamlaka ya kisheria kushiriki katika biashara za nishati na madini hapa nchini. Katika miaka ya karibuni, ushiriki huu wa dola katika tasnia ya uziduaji umetiwa nguvu zaidi na mabadiliko ya kisheria yaliyofanyika na kuunda sheria mpya kama vile Sheria ya Mamlaka ya kudumu ya Tanzania juu ya Rasilimali na utajiri wa nchi (Natural Resources (Permanent Sovereignty) Act of 2017), Tamko la uanzishwaji wa Mashirika ya Umma (the Public Corporations (Establishment Amendment) Order, 2015) na Sheria ya Mafuta (the Petroleum Act of 2015).

### **Matokeo:**

- Kwa mujibu wa ripoti za TEITI, pamoja na kupewa nguvu ya kisheria na kutengenezewa vyanzo vya mapato na serikali, kampuni zinazomilikiwa na Serikali zimekuwa zikipata hasara. Kwa mfano, ripoti ya TEITI ya mwaka 2017/18, STAMICO ilionekana kupata hasara ya kiasi cha shilingi bilioni 1.97.
- Katika ripoti hizo, mashirika haya ya serikali/dola hayakuwa na taarifa kuhusu malipo yaliyopokewa, uwekezaji mpya, hakukuwa na gawio na wala hayakulipa fedha kwa serikali.
- Taarifa hazina maelezo yoyote kuhusu ni kwa nini mashirika hayo yanaendelea kujiendesha kwa hasara. Pamoja na hasara hizo zilizopatikana, malipo ya mishahara na uendeshaji wa shughuli nyingine za kiofisi, serikali bado ililazimika kulipa kiasi cha shilingi bilioni 3.3 kwa STAMICO na shilingi bilioni 3.6 kwa TPDC.
- Ripoti ya TEITI ya mwaka 2017/18 ilionyesha kwamba ingawa baadhi ya kampuni za uziduaji zilidai kulipa kiasi cha shilingi 4, 8514 lakini malipo haya hayakuripotwa katika mifumo ya serikali na hayakuwekwa wazi kwa mlinganishi.
- Ripoti za miaka ya nyuma za TEITI zilibaini kuwepo kwa kasoro kwenye malipo yaliyokuwa yafanywe kwa TPDC na kukatolewa mapendekezo kuwa utaratibu uwekwe vizuri na kwamba baadhi ya malipo yanatakiwa kulipwa kwa Wizara ya Fedha moja kwa moja badala ya TPDC.
- Imefahamika kupitia kwa watu muhimu waliohojiwa wakati wa maandalizi ya uchambuzi huu kwamba TPDC imeanza kulipa gawio kwa serikali kuanzia mwaka 2019 na kuwa kiasi kitajulikana wakati kitakapowekwa kwenye hesabu za 2018/2019.

**Hitimisho:** Mwendelezo huu wa kupata hasara na kutoweka wazi mapato ya taasisi hizi zinazomilikiwa na serikali kunaweka mazingira ya shaka kuhusu ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwenye matumizi ya mapato haya kama inavyotakiwa kwenye viwango vya EITI na kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya TEITA ya mwaka 2015.

---

## 6.0 Mwitikio wa Serikali na Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti za TEITA

Ripoti za TEITI za kila mwaka zimeibua mambo mengi muhimu na kutoa mapendekezo kwa ajili ya utekelezaji na maboresho ya sekta ya uziduaji. Kazi kubwa ya Kamati ya Wadau (TEITI MSG) ni kuhakikisha kwamba mapendekezo yaliyotolewa yanafanyiwa kazi kwa kutekelezwa vilivyo na kasoro zilizokuwepo zinarekebisha ili zisijitokeze katika ripoti zinazofuata.

### Matokeo:

- Ripoti za TEITI zimeonyesha hesabu ambazo hazijakaa sawa zenye thamani ya mabilioni ya shilingi katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Haijulikani kama kuna ukaguzi umefanyika kuweza kubaini chanzo cha kutokaa vizuri kwa hesabu hizo na kama wahusika wa tatizo hilo wamewahi kuwajibishwa.
- Hata hivyo, kupitia ripoti ya nane ya TEITI, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliombwa kufanya ukaguzi maalumu wa kiasi cha shilingi bilioni 30.5 ambazo hesabu zilionekana kuwa na kasoro. Hadi sasa, hakuna nyaraka zozote zinazoonyesha ukaguzi huo wa CAG ulibaini kitu gani na kama kuna hatua zilichukuliwa kuweka sawa hesabu hizo. Hata hivyo, ripoti ya nane inatoa funzo kuwa CAG anatakiwa kufanya ukaguzi maalum wa kiasi hiki cha fedha cha shilingi billion 30.5.

### Jedwali: Ukaguzi wa TEITI, Matokeo na Mapendekezo ambayo hayajafanyiwa Kazi

Ripoti ya TEITI	Mapendekezo muhimu	Hali ya utekelezaji kulingana na ripoti za TEITI
Ripoti ya 2	Mafunzo ya wadau wa MSG kwa watumishi wa ofisi ya CAG na wakaguzi wa nje wa makampuni ya uziduaji juu ya EITI	Bado
Ripoti ya 4	Kuundwa na kuendelezwa kwa kanzidata ya makampuni yote ya uziduaji	Bado
Ripoti za 4 & 7	TRA kutoa nakala za stakabadhi za malipo na Taarifa za Bank	Bado
Ripoti ya 5	Tofauti isiyotatuliwa ya kiasi cha shilingi billion 8.9	Bado



Ripoti ya 7	Gawio lisilolipwa na Songas Ltd la kiasi cha dola za Marekani 479,997	Bado
Ripoti ya 7	Makampuni kutokuzingia sharia ya TEITA kwa kushindwa kutoa takwimu	Bado
Ripoti ya 7	Kuboresha hazina ya kimtandao ya Leseni za Madini iliyo na taarifa zilizo wazi kwa ajili ya umma juu ya yote yanayohusiana na leseni	Bado
Ripoti za 8 & 4	Kuboresha kanzidata katika wizara husika ili kutunza majina ya Kampuni za Uziduaji yakiwa kama walipaji na sio maajenti	Bado

## MAENEO YA TAFAKARI

### 1. Uhifadhi wa Nyaraka za Vyanzo vya Mapato kupitia Makubaliano kati ya Barrick – Serikali ya Tanzania:

Mwaka 2019, Serikali ya Tanzania na kampuni ya Barrick ziliunda kampuni ya Twiga Minerals Corporation itakayomilikiwa na wabia hao wawili kwa ajili ya kuendesha migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara. Kupitia makubaliano hayo, serikali itakuwa na umiliki wa hisa wa asilimia 16 katika migodi yote mitatu na itakuwa nusu yake ya mapato kupitia kodi, mirahaba, ushuru wa bandarini na mapato mengine ya kampuni hiyo. Utaratibu umewekwa kuhakikisha kwamba wabia hao wawili watakuwa wakigawana asilimia 50/50 ya faida inayopatikana kupitia shughuli za migodi hiyo.

Mei mwaka 2020, Barrick ililipa kiasi cha dola milioni 100 kama malipo ya awali ya fidia iliyotokana na mgogoro kati ya serikali na kampuni tanzu ya Barrick – Acacia. Mapato yaliyotokana na kampuni hii ya Twiga hayakujumuishwa katika ripoti za tisa na 10 za TEITI.

Kwa sababu ya unyeti wa uhusiano huu wa serikali na Barrick na kwa kuzingatia uzoefu wa miaka ya nyuma wa mashirika ya dola katika sekta ya uziduaji, litakuwa jambo la maana kuweka wazi nyaraka za makubaliano haya na pia kuchambua ni kwa namna mapato ya kampuni hii yatawekwa na kuangalia kwa undani katika ripoti ijayo ya TEITI.

### Uhakika wa taarifa zinazotolewa:

Pamoja na maboresho yaliyofanyika, bado kuna mapungufu katika kuaminika kwa taarifa zinazowekwa hadharani. Idadi ya taasisi zinazokubali kuwasilisha hesabu zake inaongezeka lakini nyaraka zenyewe nyingine zinaletwa zikiwa hazijasainiwa na viongozi kama sheria inavyotaka. Kampuni nyingine, kwa mfano ExxonMobil Exploration and Production Tanzania Limited zilikataa kutoa taarifa zake kwa maelezo kuwa wao wanawasilisha kupitia mwamvuli wa ORECOP na kwamba taarifa zao zote ziko huko.



## **2. Kukosekana kwa kanzidata yenye namba za mawasiliano na anuani za makazi za uhakika za kampuni za uziduaji:**

Kukosekana kwa taarifa hizi kumezifanya baadhi ya kampuni za uziduaji kuendesha shughuli zao hapa nchini pasipo hata kujulikana ofisi zao zilipo. Ripoti za TEITI hutoa pia taarifa kuhusu viongozi wa kampuni na ofisi za kazi wasiojulikana pa kuwapata. Baadhi ya kampuni zinazofanya shughuli zake hapa nchini ambazo ofisi zao za kufanyia kazi hazijulikani zilipo ni; China Development Petroleum Technology and Development Corporation, China Petroleum Pipeline Bureau (CPPB), Mubarak Gemstone Ltd, Matabe Gold Processing, GM & Company (T) Ltd, JV of CRISG and New Century Company Ltd. Orodha ya kampuni ambazo haijulikani ofisi zao zilipo imekuwa ikikua. Jambo hili linaonyesha udhaifu katika mfumo wa ufuatiliaji wa serikali na unaweza kutumika kama njia mojawapo ya kukwepa kulipa kodi. Kisheria, jambo hili linaweza kuleta shida huko mbele ya safari endapo utatokea mgogoro wa kikodi kwa sababu kuna namna tofauti ya kulipa kwa kampuni zenye ofisi Tanzania na zile zenye ofisi ughaibuni.

## **3. Utunzaji mbovu wa kumbukumbu za malipo kwa kampuni na taarifa zisizo sahihi za vyanzo vya mapato:**

Ripoti ya Saba na ya Nane ya TEITI zimeonyesha namna malipo yanayofanywa na mawakala na wawakilishi wa kampuni za uziduaji kama malipo yanayofanywa na “walipaji” pasipo kufafanua zaidi. Jambo hili linaweza kusababisha upotevu wa mapato. Katika jambo la taarifa zisizo sahihi za vyanzo vya mapato, mfano mzuri ni kampuni ya uchimbaji wa madini ya urani ya URANEX. Katika mwaka 2015/16, kampuni hiyo ilifanya malipo yaliyoelezwa kama kodi ya shirika lakini haikuwa sahihi kwa sababu ilikuwa haijaanza kazi. Kodi ya shirika hulipwa tu kwa kampuni zilizoanza uzalishaji. Kitakwimu, kumekuwa na ongezeko la mapato yanayotokana na kodi ya shirika tangu 2013/14. Kwa mfano, mwaka 2013/2014, malipo ya kodi ya shirika yalikuwa sawa na karibu asilimia 42.4 ya mapato yote ya kodi. Lakini, mwaka 2017/2018, mchango huo ulishuka kufikia kiasi cha asilimia 21.5% mwaka 20118 in 2017/18. Takwimu za namna hii zinafanya iwe vigumu kujua endapo zinaakisi ukweli halisi wa sekta ya uziduaji au kinyume chake.

## **4. Mkwamo kwenye Uwazi wa Mikataba:**

Kuhusu suala la uwazi kwenye mikataba ya kampuni zinazojihusisha na sekta ya uziduaji, serikali ilitoa taarifa mwaka 2015/2016 kwamba ilikuwa na dhamira ya kuweka wazi mikataba na makubaliano yake na kampuni za uziduaji. Mara baada ya taarifa hiyo ya serikali, kampuni mbili za kigeni; British Gas na Statoil zilitoa taarifa kwamba – ambayo ilichukuliwa kama majibu kwa serikali kwamba, kuna umuhimu wa kulinda taarifa muhimu za kampuni hizo pamoja na makubaliano yake na serikali. Ripoti za TEITI hazijaonyesha kama jambo hilo limefanayika au la. Timu ya wadau kutoka serikalini na TEITI imefanya utafiti kujua kama kampuni hizo zibaki na takwimu mpya au za zamani. Mikataba ambayo serikali imeingia mikataba ya uziduaji na kampuni kama vile Pan African Energy tayari iko mitandaoni na mtu yeyote akitaka anaweza kuiona kwenye tovuti.

*Inapatikana kupitia [www.resourcecontracts.org/countries/tz](http://www.resourcecontracts.org/countries/tz) . Hata hivyo, hii si tovuti ya serikali.*

## **5. Kuhusu suala la umiliki wa watu wenye maslahi nyuma ya kampuni:**

Kwa mujibu wa matakwa ya viwango vya EITI kupitia Kigezo 2.5 na kifungu cha 16 cha Sheria ya TEITA ya mwaka 2015, kampuni za uziduaji zinatakiwa kutaja watu wanaozimiliki katika taarifa zake. Wamiliki hawa wanatakiwa kuwa wanadamu wanaojulikana mawasiliano yao na anuani zao za makazi. Lengo la utaratibu huu ni kudhibiti vitendo vya uvunjifu wa sheria, rushwa na ukwepaji kodi katika sekta ya uziduaji. Pamoja na kuwepo kwa utaratibu huu, kampuni chache tu ndiyo zimefuata utaratibu huu.

Mfumo wa kisheria wa Tanzania ni dhaifu kutekeleza jambo hili. Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA) ndiyo wanaotakiwa kuwa na orodha ya kampuni zote zilizoajiliwa hapa nchini; zikiwa na majina yote ya kampuni, hadhi yao kisheria, anuani, mwaka iliposajiliwa na orodha ya wakurugenzi wake. Hata hivyo, BRELA haina utaratibu wa kuwa na masjala ya kuhifadhi taarifa za watu wenye maslahi na kampuni husika.

Ripoti za TEITI zinaonyesha kwamba kuna tabia iliyozoeleka ya kampuni kupuuzia uwekaji wa taarifa hizi na udhaifu kwenye kulazimisha utekelezaji. Kuna mkanganyiko kwenye tofauti kati ya wamiliki wa kampuni na watu wenye maslahi na kampuni. Katika kampuni 54 zilizofanyiwa utafiti kuhusu suala hili mwaka 2017, 31 zilitaja watu

kama wamiliki, kampuni 21 zilikuwa na mchanganyiko wa watu na kampuni kama wamiliki na kampuni 11 zilitaja kampuni kama wamiliki na kampuni 25 zilitaja watu wenye ushawishi kama watu wenye maslahi na kampuni hizo.

Katika ripoti ya TEITI ya mwaka 2017/18, ni kampuni 15 pekee, kati ya 32 zilizojaza fomu zilitaja watu wenye maslahi nazo. Kampuni 11 zilitaja kampuni nyingine kama wamiliki wake na ni kampuni mbili tu zilitaja wanadamu kama watu wenye maslahi nayo.

Kampuni kongwe na mojawapo ya kampuni kubwa za uzidujaji nchini ya Williamson Diamonds Mines iliitaja kampuni ya Wilcroft Company Ltd ya Bermuda kama mmiliki mwenye maslahi nayo. Hili ni jambo kubwa kwa sababu nchi ya Bermuda kwa muda mrefu imekuwa ikitajwa kama pepo ya wakwepa kodi kwa sababu ya sheria zake zinazochochea ukwepaji kodi kwa kisingizio cha kuwa na kodi kidogo na kufichia siri wateja wake.

Katika namna hiyohiyo, kampuni ya Neelkanth Salt Limited nayo ilisema asilimia 70 ya wenye maslahi na kampuni hiyo ni kampuni ya Pramukh Associates Ltd ya Mauritius huku kampuni ya Tanzania China International Mineral Resource Limited ikiandika kwamba asilimia nane ya wamiliki wake ni kampuni ya Sichuan Hongda Group.

Mifano hii ya kutofuatwa kwa sheria inaonyesha kwamba bado kuna changamoto kubwa katika kuhakikisha taarifa muhimu kuhusu wamiliki na wenye maslahi kwenye kampuni za uzidujaji. Hili ni jambo ambalo MSG inatakiwa kulifanyia kazi vya kutosha.

Bunge la Tanzania lilipitisha Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 mnamo Juni 15 mwaka huu. Pamoja na mambo mengine, sheria hiyo imefanya marekebisho katika sheria za Utakatishaji Fedha, Kodi ya Mapato na Sheria ya Makampuni kwa kuingiza tafsiri mpya kuhusu wenye maslahi na kampuni na masjala yao. Tafsiri hiyo na taarifa zinazohitajika kwa ajili ya masjala ya wenye maslahi inaendana na vigezo vya TEITI vya mwaka 2019 na ni jambo zuri kwamba sasa sheria imeliweka jambo hili vizuri.

Hii ni taarifa muhimu kwa sababu ukosefu wa msingi wa kisheria wa jambo hili ulikuwa kikwazo kwa TEITI kupata taarifa ilizozitaka kuhusu jambo hili. Sasa kuna fursa kwa TEITI na BRELA kufungua mlango wa ushirikiano katika suala zima la upatikanaji wa taarifa za wamiliki na wenye maslahi na kampuni za uzidujaji. TEITI imepanga kukutana na wadau muhimu, zikiwamo kampuni na serikali, kwa ajili ya kuandaa mafunzo na uwezeshaji kuhusu eneo hili.

## **6. Mgawanyo na Uhamishaji wa Mapato:**

Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 ilitoa ruhusa ya kuhamisha mapato baina ya taasisi za kitaifa na za ngazi za chini na pia kutoa ruhusa ya kufanya ukaguzi wa matumizi. Uhamishaji wa mapato yatokanayo na uzidujaji unafanyika tofauti na mapato mengine. Mapato kutoka vyanzo vyote hukusanywa na kuwekwa kwenye mfuko mkuu wa serikali na hutumiwa na taasisi za serikali kwa maelekezo ya Serikali Kuu.

Kwa mujibu wa Wizara ya Fedha na Mipango, mapato kutoka katika sekta ya uzidujaji huingizwa katika bajeti ya taifa kupitia katika taarifa rasmi za kifedha kwenye vitabu vya mapato. TEITI imeripoti kwamba TRA ilikua kwenye mchakato wa kuhifadhi taarifa za mapato yote kama inavyotakiwa na IMF. Hata hivyo, hadi sasa, hakuna mwongozo rasmi ambao umetolewa kuhusu ni kwa vipi fedha zinazopatikana kupitia sekta ya uzidujaji zinavyotumika au kama ni fungu tofauti kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Hakuna taarifa rasmi inayoonyesha kama TRA wametekeleza suala hilo la maelekezo ya matumizi ya fedha za uzidujaji kama walivyohidi miaka mitano iliyopita.

## **7. Utekelezaji dhaifu wa Mapendekezo ya Ripoti za Nyuma.**

Uchambuzi huu umebaini kwamba hili ndilo tatizo kubwa la udhaifu katika ufuatiliaji wa mapendekezo ya ripoti. Kwa mfano, katika ripoti ya nane, kiasi cha shilingi bilioni 30.5 kiliripotiwa kuwa hesabu zake hazijakaa vizuri lakini hadi sasa hakuna maelezo ya kufuatilia kuhusu nini kimefanyika. Uchunguzi wa CAG uliofanyika kutazama



jambo hili haujulikana matokeo yake yalikuwa nini. TEITI ilikuwa imepanga kuchapisha muhtasari wa matokeo ya uchunguzi huo mwaka huu. TEITI planned to publish a summary of the findings in 2020. Ripoti za TEITI huwa zinaweka bayana mambo ya msingi ya kufanyiwa kazi na mambo ambayo yamefanyiwa kazi kutoka ripoti za nyuma. Pengine, kama kungekuwa na aina fulani ya adhabu na vikwazo kutoka EITI kwa nchi ambazo hazifuati vigezo, kungesaidia mapendekezo kufuatwa.

#### **8. Taarifa isiyojitosheleza kuhusu manunuzi na misaada.**

Ripoti ya 10 ya TEITI iliweka taarifa kuhusu uwajibikaji wa makampuni kwa jamii na manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka ndani ya nchi yaliyofanywa na kampuni za uziduaji kwa mujibu taratibu. Hata hivyo, mchanganuo rasmi wa kimahesabu kuhusu manunuzi na malipo haya haupo. Taarifa kuhusu manunuzi ya ndani kutoka kwa kampuni kubwa kama Geita Gold Mine hazipo kabisa. Taarifa kamili kuhusu misaada na michango kwa jamii inayofanywa na kampuni hizi haiwekwi katika namna ambayo mtu anaweza kulinganisha na mapato halisi ya kmapuni. Kwa sababu hiyo, ni vigumu kufahamu kama michango, manunuzi na misaada hiyo ni mikubwa kiasi gani kulinganisha na kile ambacho kampuni hizi zinapata.

#### **9. Kupunjwa kwa mchango wa sekta ya Gesi na Mafuta:**

Ingawa sekta hii inakua vizuri, takwimu zilizopo hazitoa picha hiyo na huenda ziko chini kuliko halisi ilivyo. Kwa mfano, mirabaha ya gesi iliyolipwa kwa TPDC haikuandikwa popote kwenye ripoti ya TEITI ya mwaka 2015/2016. Kuna uwezekano wa kupata mapato kutoka makinikia ya gesi lakini fedha hizo hazionekani katika ripoti ya TEITI. Hakuna ukaguzi wowote uliofanywa kwenye Mfuko wa Gesi na Mafuta ambao unaelezwa kuanza kupokea fedha kutoka TPDC kama mojawapo ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya TEITI ya mwaka 2014/15 (Ripoti ya Nane, Uk 8).

#### **10. Hasara za muda mrefu za mashirika ya serikali:**

Pamoja na ukubwa wake na nguvu ya serikali ndani yake, mashirika yanayomilikiwa na serikali yamekuwa yakitangaza kupata hasara kila mwaka. Ripoti za TEITI zinaonyesha ugumu wa kupata taarifa za hesabu za mashirika haya na taasisi kama STAMICO na TPDC zimekuwa na hesabu zinazoonyesha mapungufu katika uwajibikaji. Serikali bado imeendelea kutumia kiasi kikubwa cha fedha kuhudumia mashirika yake kwa gharama za uendeshaji ikiwamo kulipa mishahara ya wafanyakazi. TRA ambayo ina jukumu la kukusanya mapato ya uziduaji imeendelea kuwa mojawapo ya taasisi ambazo ripoti zake zina mapunguzi ya kihesabu. Ripoti za mwaka 2016/17 na 2017/18 zimefanikiwa kupata hesabu zilizokaguliwa za mashirika ya serikali kama vile STAMICO, STAMIGOLD na TPDC. Kuanzia mwaka 2019, TPDC na STAMICO zimeanza kulipa gawio kwa serikali. STAMICO ililipa shilingi bilioni moja mwaka 2018/19 na shilingi bilioni 1.1 mwaka 2019/20.

#### **11. Mapitio ya Vigezo vya Ukaguzi:**

Kiwango cha chini cha ukaguzi kwa ajili ya kuingizwa kwenye ripoti za TEITI kimeongezeka kutoka kiwango cha chini cha shilingi milioni 150 mwaka 2008/09 hadi shilingi milioni 900 mwaka 2017/18. Kiwango hiki cha chini huwekwa na MSG kutokana na utafiti ambao hufanywa rasmi kwa ajili hiyo huku kigezo kikubwa kikiwa ukubwa wa mapato yanayotakiwa kufanyiwa ukaguzi. Ziko kampuni ambazo hazikufikia kiwango hicho lakini bado taarifa zake zilichapishwa. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, ilibainika kwamba kwa kiwango hicho kilichopendekezwa, kampuni ambazo huchangia asilimia 95.52 (2016/17) na asilimia 94.06 (2017/2018) ya mapato yote ya serikali kwenye sekta ya uziduaji yatakuwa yameingizwa kwenye ripoti kwa mwaka 2017 na 2018 mtawalia.

Kwa sababu hiyo, kupitia utaratibu huu, sehemu kubwa ya kampuni zinazolipa kodi kubwa huingizwa katika ripoti hiyo. Kwa nyongeza, kwa kuishibisha ripoti, EITI huchagiza pia kampuni nyingine ambazo hazijafikia vigezo kutoa taarifa zao pia. Hata hivyo, jambo hili linatakiwa kutazamwa upya. Kwa kuangalia mifano ya nchi nyingine kama Zambia, utaratibu huu wa kuweka vigezo na ukomo, unaweza kusababisha sehemu kubwa ya walipa kodi kukwekwa nje ya wigo. Suala hili la ukomo linaweza kusababisha serikali ikakosa kodi muhimu ambayo inaweza kusaidia; hata kama kiwango cheneyewe kinaweza kuwa asilimia moja tu.



**12. Kukosekana kwa muunganiko baina ya ripoti ya hesabu za TEITI na hali halisi kwa wananchi**

Ripoti hizi za hesabu za TEITI bado zinaonekana kuwa na mwonekano wa kitaifa na mambo makubwa makubwa lakini zikiwa zinakosa hali ya kugusa maisha ya watu katika jamii. Jambo hili limesababisha kuwepo kwa pengo katika mashirikiano baina ya ngazi ya kitaifa na katika ngazi za chini. Ripoti za TEITI zilijaribu kuangalia eneo la malipo yanayofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na ilifanikiwa kufanya mapitio ya hesabu zake. Hesabu hizi ni zile za kodi za huduma na nyingine ndogondogo zinazolipwa katika ngazi za chini.

Ripoti hizo zilijumuisha pia taarifa kuhusu uzalishaji na mauzo, huduma kwa jamii na malipo ya leseni kwa seriali na mengine yanayofanywa na kampuni hizi. Lengo la kufanya hivi ni kujaribu kuzipa jamii ambako shughuli za uziduaaji zinafanyika taarifa za kutosha kuhusu sekta hii. Zaidi, uwazi katika malipo na mapato ni muhimu kwa vile unajenga mazingira wezeshi kwa uwekezaji, unajenga kuaminiana na jamii husika na kuzipatia kampuni hizi kibali cha kijamii kuendelea na shughuli zake katika maeneo hayo.

Hata hivyo, bado kuna tatizo kwenye eneo hili la uhusiano na jamii hizi na namna taarifa hizi zinavyowafikia wananchi. Inawezekana kwamba tatizo ni kwamba mchakato unaotumika sasa wa kuandaa taarifa hizi za TEITI na mtindo wa uandishi haukuwa umelenga jamii za chini. Lakini, kwa sababu ya namna sekta ya uziduaaji ilivyo muhimu na inavyogusa maisha ya wananchi moja kwa moja, ni muhimu kwa MSG kufikiria kutengeneza mfumo mpya wa uandaaji wa ripoti ambao utasaidia kujenga uhusiano mzuri na jamii.

---

<sup>18</sup><https://www.barrick.com/English/news/news-details/2019/The-Launch-of-Twiga-Minerals-Heralds-Partnership-Between-Tanzanian-Government-and-Barrick-/default.aspx>

---

## Mapendekezo

---

### Kwa TEITI, MSG na Serikali

1. Kufanya mabadiliko katika mfumo wa kuandika ripoti ya malipo na kuweka kipengele kitakachoonyesha taarifa za mafanikio na changamoto ambazo zinaweza kuchukuliwa na kufanyiwa kazi na wadau wa ndani kwa lengo la kufanyiwa kazi kwenye harakati na uchechemuzi.
  2. Kuongeza mawanda ya ukusanyaji wa rasilimali ili kuongeza wigo wa ushiriki na maeneo na kuifanya TEITI iendelee kuwa na manufaa kwa wadau wake.
  3. Kurasmisha na kutanua wigo wa mikutano ya wadau wa uziduaji ili ijumuishe asasi nyingi zaidi za kiraia kuondoa zile zilizo kwenye CSO-MSG.
  4. Kuanzisha mabadiliko ya kitaasisi ndani ya TRA ili kuhakikisha malipo ya sekta ya uziduaji yanaripotiwa kwa usahihi.
  5. Kwa sababu TPDC inaelezwa kuwa imeanza kulipa mrabaha kwenye Mfuko Mkuu wa Gesi na Mafuta, TEITI na MSG sasa zinapaswa kuanza kufanya ukaguzi wa mfuko huo.
  6. Kuweka mfumo mzuri wa ufuatiliaji wa mambo ambayo yalionyesha matatizo kwenye ripoti ya TEITI. Ripoti ya CAG iliyofanyia kazi matatizo hayo ni muhimu iwekwe wazi pia. Hili ni muhimu kwa sababu ya kujenga uwajibikaji na kujifunza kwa wale wanaolipa na kulipwa.
  7. Kuanzisha kanzidata yenye taarifa sahihi za anuani za ofisi zilipo kampuni za uziduaji. Taarifa kuhusu kampuni ambazo ofisi zake hazijulikani zilipo hata baada ya ukaguzi zinatakiwa kuwekwa hadharani.
  8. Kufanyika kwa ukaguzi wa hesabu za makinikia ya gesi iliyozalishwa na kuuzwa kutoka katika vitalu vya Songosongo na Mnazi Bay katika kipindi cha miaka 16 iliyopita (2004-2020).
  9. Kuwepo kwa takwimu rasmi za hesabu kuhusu misaada ya kijamii na manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanywa na kampuni za uziduaji.
  10. Kuanzisha utaratibu wa kutoza faini kwa kampuni za uziduaji ambazo zimejaza fomu za kuweka taarifa zake za hesabu katika namna ambayo haiendani na matakwa ya kisheria kupitia Sheria ya TEITA ya mwaka 2015.
  11. Kufanywe mafunzo kwa kampuni za uziduaji kuhusu suala zima la watu wenye maslahi na kampuni zao na hasa wenye ushawishi kisiasa kupitia ripoti za TEITI. Kampuni za Williamson Diamonds na Neelkath Salt Ltd zinatakiwa kuweka wazi ni watu gani hasa wanamiliki kampuni hizo ambao wana makazi Bermuda na Mauritius.
  12. Kuanzisha utaratibu wa kuweka wazi taarifa zote za malipo kwa wakati na kwa usahihi ili kuepusha kutoa taarifa zisizo sahihi au zilizopitwa na wakati.
-



13. Kuwasiliana na kampuni zote za uziduaji na kuzitaka zitoe taarifa rasmi, kila moja, kuhusu msimamo wake kwenye suala la uwekaji wazi wa mikataba.
14. Kumtaka waziri kuweka utaratibu wa kuandaa ripoti makini kuhusu hesabu zilizofanyiwa kazi na kuchunguzwa na CAG kama inavyotakiwa na sehemu ya 18 na 19 ya Sheria ya TEITA yam waka 2015.

### **Kwa makampuni**

Uwekaji wazi wa taarifa za mapato umeonyesha kwamba mara nyingi serikali hutoa taarifa kuonyesha imepata kidogo kuliko kile kinachoelezwa kulipwa na kampuni za uziduaji, tunazishauri kampuni hizi kuweka utaratibu wa kuweka taarifa zao malipo wanayofanya kwa serikali kwenye tovuti zao.

1. Suala la uwekaji wazi wa mikataba linasuasua kwa sababu baadhi ya kampuni za uziduaji bado zinapinga, ni muhimu kwa kampuni zote za uziduaji kutoa taarifa kwa umma kuhusu msimamo wao kwenye suala hili.
2. Kampuni zote za masuala ya gesi ziweke hadharani risiti za mauzo ya makinikia ya gesi, kama yanazalishwa, katika kipindi cha miaka 16 iliyopita.
3. Hesabu zote za malipo yanayofanywa na kampuni za gesi ziwekwe hadharani ili mchango wa sekta ya mafuta na gesi nao ufahamike.
4. Taarifa zote muhimu kuhusu malipo yaliyofanyika kwa watoa huduma na biashara wa kampuni za uziduaji na misaada yote kwa jamii iwekwe hadharani.
5. Katika kampuni zote za uziduaji, kuwe na mtu mmoja mwenye jukumu kuhakikisha ana taarifa zote muhimu za TEITI ili mar azote kuwa na taarifa sahihi.

### **Kuhusu Asasi za Kiraia na Wawakilishi wa Wadau kwenye MSG**

1. Kuna tatizo la uratibu miongoni mwa asasi za kiraia zinazojihusisha na sekta ya uziduaji kiasi kwamba zipo nyingine zimeanza kujitenga. Tunapendekeza Hakirasilimali na asasi nyingine za kijamii kuongeza nguvu katika eneo la uratibu, kujengea wanaharakati uwezo na kubadilishana maarifa na watu wapya wanaoingia katika harakati za kupambania masuala ya uziduaji.
2. Kuna haja ya kuomba kuongezeka kwa muda wa mashauriano baina ya wakaguzi wa taarifa wa EITI, wakaguzi wa hesabu wa TEITI na asasi za kiraia ili kupata taarifa rasmi na nyingi kwa wakati mmoja. Kwa sasa, majadiliano ni kati ya MSG na wawakilishi wa CSO pamoja na wadau wengine muhimu.
3. Wakati umefika kudai kwamba kuanzia sasa, taarifa za ukaguzi uliofanywa na CAG katika maeneo yaliyokuwa na shida ziwekwe katika tovuti ya TEITI na pia waziri mwenye dhamana ya uziduaji aiwasilishe bungeni kama yalivyo matakwa ya Sheria ya TEITA ya mwaka 2015.